

MSUMBII

MICHANGO imekuwa ikiendelea kutolewa na wananchi katika sehemu mbalimbali nchini kutunisha mfuko wa kuwasaidia wananchi wa Msumbiji wanaokabiliwa na mapambano dhidi ya magaidi wa MNR wanaosaidiwa na Afrika Kusini.

Huko Arusha wanamgambo wa kata za Duru na Riroda katika wilaya ya Babati wamechanga jumla ya sh. 10,554 kuwasaidia wananchi wa Msumbiji, SHIHATA ilieleza juzi.

Mchango huo ulikabidhiwa jana kwa Mkuu wa Wilaya ya Babati, Luteni Kanali Anatoli Tarimo, alipofungua mafunzo ya awali katika kijiji cha Riroda yanayowashirikisha zaidi ya wanamgambo 800.

Mjini Dar es Salaam wanachama wa tawi la Hoteli la Bahari Beach wametoa sh. 6,800 kwa ajili ya kuwasaidia wananchi hao.

Akipokea mchango huo kwenye mkutano wa wanachama hao mwenyekiti wa wilaya ya Kinondoni Ndugu Godfrey Makaya aliwataka wanachama wa CCM kuzidisha mshikamano katika kusaidia mapambano kusini mwa Afrika.

Uhuru 31/8/87 p. 5